




## Hadithi ya Malik

### Malik's story

 LIDA Italia

 Vilius Aistis Vilimas

 Jacob Haule

 4

 Kiswahili sw / English en



Jina langu ni Malik na nina umri wa miaka 39. Nilizaliwa huko Afghanistan. Dini yangu ni tofauti na dini kuu ya Afghanistan.

...

My name is Malik and I am 39 years old. I was born in Afghanistan. My religion is different from the main religion in Afghanistan.



Kwa miaka mingi, watu wa dini yangu wamekuwa wakiteswa. Hii imekuwa ni changamoto kubwa sana kwa familia yangu.

...

For many years, people who belong to my religion have been persecuted. This has been very difficult for my family.



Miaka michache iliyopita kulikuwa na vita. Nilikuwa na hofu kwamba ningeuwawa. Niliacha familia yangu na kwenda Ulaya na kuanza maisha mapya.

...

A few years ago there was a war. I was afraid I would be killed. I left my family to go to Europe and start a new life.



Nilitembea kwa kilomita nyingi na wakati mwingine sikuwa na chakula wala sehemu ya kukaa. Baadhi ya watu niliosafiri nao walifariki.

• • •

I walked for many kilometres. Sometimes I had no food and nowhere to stay. Some of the people I travelled with died.



Hatimaye nilifika Ulaya. Nilikutana na watu kutoka kwenye nchi yangu ambao walinisaidia. Sifahamu ningelifanya nini bila wao.

...

Finally I arrived. I met some people from my own country who helped me. I do not know what I would have done without them.



Nilianza kujifunza lugha, lakini ilikuwa ngumu. Nilijua kwamba kuongea lugha hiyo ilikuwa muhimu katika kupata kazi.

...


I started to learn the language, but it was hard. I knew that speaking the language was important to get a job.



Nilijifunza kwa miaka kadhaa, cha kwanza kabisa ni kujifunza lugha. Ilikuwa ngumu, lakini ninafurahi kujifunza mambo mapya.

• • •

I studied for several years, at first to learn the language. It was hard, but I enjoy learning new things.



Baada ya kujifunza, nikaanza kufanya kazi. Kwanza nilifanya kazi katika mgahawa, na kisha nikawa mwalimu kwa sababu ninataka kusaidia wengine.

• • •

After studying I started working. First I worked in a restaurant, and then I became a teacher because I want to help others.



Ninatumaini kuwa siku moja nitarejea Afghanistan. Watu wengi huko wanahitaji msaada na ninataka kuwasaidia.

• • •

I hope to go back to Afghanistan one day. Many people there need help, and I want to help them.



## LIDA Stories


[lidastories.net](http://lidastories.net)

### Hadithi ya Malik

#### Malik's story

 LIDA Italia

 Vilius Aistis Vilimas

 Jacob Haule (sw)

